

HUDUMA NYINGINEZO

- Kuhasi nguruwe dume madogo am-bao hawahitajiki kwa uzazi.

HITIMISHO

Ili kufuga kwa mafanikio, wafugaji wanashauriwa kuwaona wataalam wa mifugo walio karibu nao ili kupata ushauri juu ya ufugaji bora wa nguruwe.



**Ufugaji bora, kinga na
chanjo muhimu za
nguruwe**

Imetolewa na
Kliniki ya Mifugo
Kitivo cha Tiba ya mifugo
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
P. O. Box 3015
Chuo Kikuu MOROGORO
Simu: 0232 60 1495



UTANGULIZI

Nguruwe ni mnyama ambaye ni rahisi kufuga na hana mahitaji makubwa. Huweza kufugwa kwenye eneo dogo, hula aina nyingi za vyakula, huzaana kwa wingi na akipewa chakula bora na cha kutosha hukua haraka na kufikia uzito wa kuchinjwa.

Kuna aina/kabila nyingi za nguruwe kama vile nguruwe wa kienyeji, nguruwe wa kisasa na chotara.

Mbali na kutoa nyama, nguruwe pia hutupa mbolea, manyoya (kwa ajili ya kutengenezea brashi) na pia mifupa yake hutumika kama chakula cha mifugo (bone meal)

UTUNZAJI

NYUMBA

Nguruwe wanahitaji banda zuri lenye kuta, sakafu na paa madhubuti. Pia nyumba ya nguruwe inahitaji nafasi ya kutosha, hewa na mwanga. Vilevile ni lazima kuwe na sehemu ya chakula na maji. Usafi katika banda la nguruwe ni muhimu sana.

CHAKULA

Nguruwe hula aina nyingi za vyakula. Kwa mfano pumba, majani, damu, dagaa, madini pamoja na mabaki ya chakula cha binadamu. Nguruwe wapewe chakula kingi cha kutosha ili kuwawezesha kujenga mwili na kuwa na kinga ya maradhi. Pia nguruwe wanahitaji maji safi ya kunywa. Nguruwe wadogo ni vema wanyonye kwa mama yao.

MAGONJWA MUHIMU YA NGURUWE

Nguruwe huweza kupata magonjwa yafuatayo kirahisi:-

- Minyoo
- Ugonjwa wa ngozi (ukurutu)
- Kuharisha
- Ukosefu wa madini

KINGA DHIDI YA MAGONJWA

Nguruwe wapewe dawa ya kuua minyoo kila baada ya miezi 3. Tatizo la minyoo ni kubwa sana hasa kwa nguruwe wadogo.

Ugonjwa wa ngozi udhibitiwe kwa kuwatibu nguruwe wanaoonyesha dalili.

Nguruwe wadogo (chini ya wiki mbili) wachomwe sindano ya madini ya chuma. Pia katika mchanganyiko wa chakula cha nguruwe ni lazima kuwe-kwe madini.

Usafi wa banda, sehemu za chakula na maji ni muhimu ili kuweza kudhibiti magonjwa mbalimbali ikiwemo kuaha-ra.